**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI KWA NIABA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO CHA 77 CHA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU, KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA ARUSHA (AICC)**

**TAREHE; 20 OKTOBA, 2023**

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya
Afrika ya Haki za Binadamu na Watu;**

**Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya
Afrika ya Haki za Binadamu na Watu;**

**Wahesimiwa Makamishna wa Tume ya
Afrika ya Haki za Binadamu na Watu;**

**Waheshimiwa Wawakilishi wa Nchi
Wanachama wa Umoja wa Afrika,**

**Viongozi Mbalimbali wa Nchi na Serikali,
Waheshimiwa Mabalozi,**

**Wadau wa Mbalimbali wa Maendeleo,**

**Waheshimiwa Wenyeviti na Makamishna wa
Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu,**

**Washiriki Kutoka Taasisi Zisizo za Kiserikali**

**Wananchi Mliopo,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana,**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia neema ya uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo katika hafla ya ufunguzi wa kikao cha 77 cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).

Kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda nikupongeze Mheshimiwa Prof. Remy Ngoy Lumbu, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Watu kwa uongozi wako imara katika kuiongoza taasisi hii muhimu ya Umoja wa Afrika, Taasisi ambayo inalinda, inakuza na kuendeleza haki za binadamu na watu katika Bara la Afrika.

Pia, niwapongeze Makamishina wote wa Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambao mnashirikiana pamoja katika kuimarisha haki za binadamu na watu katika bara la Afrika. **HONGERENI SANA.**

**Ndugu Washiriki**,

Kikao hiki ni matokeo ya ziara ya Mwenyekiti wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu aliyoifanya nchini Tanzania tarehe 30 Januari, 2023, ambapo pamoja na masuala mengine yaliyojadiliwa, pia aliomba mkutano huu ufanyike hapa Tanzania. Hivyo, kwa niaba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natumia fursa hii kuwashukuru kwa uamuzi wenu wa kufanya kikao cha 77 cha Kawaida cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu hapa nchini Tanzania**.**

**Ndugu Washiriki**,

Kwa niaba ya Serikali na Watanzania wote, napenda kuwakaribisha viongozi na waalikwa wote kutoka nchi mbalimbali wakiwemo; Waheshimiwa Mawaziri; Mabalozi na Viongozi wa Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu na Asasi za Kiraia (AZAKI); pamoja na wawakilishi wa Serikali na makundi mbalimbali kutoka Bara la Afrika.

Nimejulishwa kuwa katika mkutano huu, yatajadiliwa masuala mbalimbali ikiwemo hali ya haki za binadamu katika bara la Afrika, taarifa za kazi za Makamishna pamoja na taarifa za mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu Afrika. Ni matumaini yangu kuwa taarifa hizi zitatoa tathimini ya hali halisi ya haki za binadamu na kutoa mapendekezo yatakayosaidia kupata mbinu za kukabiliana na changamoto

zitakazoainishwa. Aidha, naamini kwamba washiriki watapata fursa ya kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusiana na masuala yatakayojitokeza katika taarifa zitakazo wasilishwa.

**Ndugu Washiriki**,
Nafahamu kuwa kikao hiki kilitanguliwa na majukwaa ya Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu zipatazo **46** na Asasi za Kiraia takribani **210** kutoka Bara la Afrika. Taasisi hizi ni wadau muhimu katika masuala ya ulinzi, utetezi na uhifadhi wa haki za binadamu barani Afrika. Nakupongezeni sana kwa kuona umuhimu wa kuandaa majukwaa ya Taasisi na Asasi hizo.

**Ndugu Washiriki**,
Ni vyema ikakumbukwa kuwa kila mwaka ifikapo tarehe 21, Oktoba, Bara la Afrika linaadhimisha Siku ya Haki za Binadamu Afrika ambapo kauli mbiu ya mwaka huu wa 2023 ni **"*Kuimarisha na Kuendeleza Utamaduni wa Haki za Binadamu kwa Nyakati zijazo*".** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na nchi zote za Bara la Afrika na wadau wengine wa haki za binadamu katika maadhimisho haya muhimu. Nitoe wito kwa Serikali mbalimbali na Taasisi za haki za binadamu kuendelea kuchukua hatua za kuimarisha ulinzi na utetezi wa haki za binadamu na kushughulikia kikamilifu changamoto zilizopo.

**Ndugu Washiriki**,

Kwa hakika, kauli mbiu ya siku ya haki za binadamu ya Afrika ya mwaka huu, inanishawishi kuwakumbusha ndugu zangu kutoka Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu, AZAKI na wadau wengine wote mliopo hapa kuwa haki za binadamu tunazozitetea ziwe zinaendana na kauli mbiu hii. Kwa ujumla, Bara la Afrika na Tanzania kwa umahususi wake tunaheshimu haki za binadamu kwa kuzingatia utamaduni, maadili na tunu zetu kama Waafrika.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza na kusimamia haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Katika katiba yetu, haki za binadamu zimeainishwa kuanzia Ibara ya 12 hadi 24 lakini pia Katiba yetu kuanzia Ibara ya 25 hadi 30 imeainisha wajibu wa kila raia. Katika kuhakikisha tunazilinda haki za binadamu na watu, hapa Tanzania tulianzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Taasisi hii ya kitaifa, tumeianzisha kwa lengo la kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu nchini.

**Ndugu Washiriki**,

Hapa nchini, jitihada mbalimbali zimechukuliwa na Serikali ili kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kutekelezwa kwa mujibu wa Mikataba ambayo Tanzania ni mwanachama. Kwa kiasi kikubwa, jitihada hizi zimeboresha hali ya upatikanaji wa haki mbalimbali ikiwemo haki ya

usawa mbele ya sheria, afya, elimu, maji na mazingira safi, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kuabudu, ajira, haki ya kumiliki mali na uhuru wa vyombo vya habari. Kwa taarifa ni kwamba, kutokana na uhuru huo, hivi sasa Tanzania ina vyombo vya habari vingi vikiwemo redio **210**, televisheni **56**, magazeti **288** pamoja na mitandao mbalimbali ya kijamii. Pia, tumefikia hatua kubwa ya kuimarika kwa uhuru wa kidemokrasia, haki za wanawake, watoto na watu wenye ulemavu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

**Ndugu Washiriki**,

Sote tunafahamu kuwa suala la ulinzi na uhifadhi wa haki za binadamu katika bara la Afrika kwa jumla, bado kwa kiasi fulani linakabiliwa na changamoto. Miongoni mwao ni mapinduzi ya Serikali zilizo madarakani, vita vya wenyewe kwa wenyewe, mila na desturi zisizofaa, ukatili wa kijinsia, athari hasi za utandawazi na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu haki zao. Natumia fursa hii kutoa wito kwa nchi na Serikali zote wanachama wa Umoja wa Afrika kuchukua hatua stahiki katika kukabiliana na changamoto hizo.

**Ndugu Washiriki**,

Kwa hakika, changamoto na majanga mbalimbali ambayo bara letu linapitia, wahanga wake wakubwa ni wanawake na watoto. Kwa kutambua hilo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua katika kutatua migogoro mbalimbali na

kutekeleza kwa vitendo ***Tamko la Dar es Salaam*** kuhusu Amani, Usalama, Demokrasia na Maendeleo katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Kwa mfano hivi sasa Tanzania inashiriki katika jeshi la Umoja wa Mataifa Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (*Stabilization Mission*) na Jeshi la Kulinda Amani (MONUSCO).

Aidha, katika kuepusha uvunjifu wa haki za binadamu unaotokana na vita, kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania inashiriki katika Jeshi la pamoja la kulinda amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Pia, Tanzania kwa muda mrefu imeshiriki katika ulinzi wa amani katika nchi mbali mbali ikiwemo huko Darfur Sudan na Visiwa vya Comoro. Naona fahari kwa Majeshi yetu kwa kazi yao nzuri wanayoifanya. Nitoe wito kwa nchi zetu za Afrika kuendelea kushirikiana katika kuyakabili matukio mbalimbali yanayohitaji msaada wa kibinadamu katika Bara letu.

**Ndugu Washiriki**,

Kwa mara nyingine, nachukua fursa hii kutoa rai kwa waalikwa kushiriki kikamilifu katika Kikao cha Kawaida cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa kutoa michango ya mawazo, ufafanuzi na mapendekezo kwa madhumuni ya kuboresha hali ya haki za binadamu katika Bara la Afrika.

**Ndugu Washiriki,**

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuwakaribisha tena washiriki wote hapa Tanzania ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kuvitembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo hapa Tanzania Bara na kule Zanzibar. Nahitimisha maelezo yangu kwa kuwatakia kikao chema na mafanikio. Nimefurahi kusikia kuwa mtakuwa na siku 11 katika vikao vya washiriki wote (*public session*) na siku 9 za vikao vya Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (*private session*). Napenda kuwahakikishia kuwa, Tanzania ina amani na hali ya usalama katika Mkoa huu wa Arusha na nchi nzima kwa ujumla. Niwatakie kila la kheri ili muyafikie malengo yaliyokusudiwa katika kikao hiki.

**BAADA YA KUSEMA HAYO SASA NATAMKA KUWA KIKAO CHA 77 CHA TUME YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU KIMEFUNGULIWA RASMI**

**Asanteni kwa kunisikiliza.**